



Mamlaka ya kuzuia Rushwa na uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) imemkamata ndugu KHAMIS HAJI MUSSA Mkaazi wa MICHENZANI Unguja mwenye umri wa miaka 62 kwa tuhuma ya kuomba na kupokea rushwa kitendo ambacho ni kinyume na kifungu cha 42 na 43 vya sheria nambari 1/2012.

Akizungumza na waandishi wa Habari Afisa wa Mamlaka ya kuzuia rushwa na Uhujumu Uchumi Ndugu YUSSUF JUMA SULEIMAN katika ofisi za ZAECA kwa niaba ya mkuu wa uchunguzi na operesheni amesema baada ya kupokea taarifa kutoka kwa wasiri wao ukaandaliwa mtego mnamo majira ya saa sita 12:00 mchana siku ya tarehe 6/2/2020 na ndipo alipo kamatwa.

Amesema Suleiman Mzee huyo amekamatwa nyumbani kwake akiwa na vielelezo tofauti, kama vile vyeti vya kumalizia masomo, vyeti vya kuzaliwa ,vitambulisho vya mzanibar pamoja na pesa taslim kwa ajili ya kuwapatia vijana ajira.

Sambamba na hayo afisa huyo ametoa wito kwa Umma kufuata sheria wakati wanapotafuta huduma, pia kuripoti vitendo vya rushwa kwa kupiga nambari 113 pindi wanapo pata kadhia kama hiyo.